

Athari za Kifonolojia za Lugha za Kinailotiki kwa Kiswahili: Mifano kutoka Kenya

James Omari Ontieri
Chuo Kikuu cha Maasai Mara

Ikisiri

Lugha ya Kiswahili ina mfumo wa kifonolojia ambao una upekee unapolinganishwa na lugha nyinginezo. Tunapochunguza mfumo huu na kuulinganisha na ule wa lugha za Kinailotiki kunadhihirika tofauti anuwai. Makala haya yanalenga kuchanganua namna tofauti kati ya mifumo ya kifonolojia husika inavyochangia makosa ya kimatumizi wakati wazawa wa Kinailotiki wanapoandika kwa Kiswahili. Data ya makala haya inatokana na uchanganuzi wa mawasiliano andishi ya wanafunzi wa shule za upili katika shule teule wilayani Nakuru, Kenya. Wanafunzi husika waliandika insha moja ambayo ilichanganiliwa ili kuibuka na data hii. Makosa yanayotokana na athari za kifonolojia yamechanganuliwa huku njia sahihi ya kuyaandika maneno husika ikionyeshwa. Uchanganuzi huo uliongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi Makosa (Corder, 1967). Matokeo ya uchunguzi huu yatawasaidia wanafunzi wa taaluma ya Kiswahili katika kuzua mikakati ya kupunguza makosa ya aina hiyo katika maandishi yao. Aidha, walimu watanufaika na matokeo ya utafiti huu katika harakati za kuwaelekeza wanafunzi kuhusu matumizi sahihi ya Kiswahili hasa kimaandishi. Kuhusiana na taaluma ya Kiswahili kwa jumla, matokeo ya utafiti huu yatachangia kuweka wazi masuala muhimu ya kuchunguzwa katika uwanda wa uchanganuzi makosa.

Maneno Muhimu: Fonolojia, athari, nailotiki, Kiswahili

Utangulizi

Lugha zinapotagusana katika jamii yoyote ile kuna uwezekano mkubwa wa kuathiriana katika vipengele mbalimbali. Athari za aina hii huweza kuwa za upande mmoja au za pande mbili husika. Tunachunguza athari za kifonolojia zinazojitokeza katika kazi andishi ya wanafunzi wazawa wa jamii-lugha anuwai za Kinailotiki wanapowasilisha ujumbe kwa Kiswahili. Kimsingi, watafitiwa ambao tayari wanajua lugha yao ya kwanza, huitegemea wakati wanapojifunza

lugha ya pili. Kwa mujibu wa Richards (1974), tajriba ya mwanafunzi katika lugha ya kwanza, huhamishiwa katika lugha ya pili kwa lengo la kurahisisha ujifunzaji wake. Uhamishaji wa aina hii husababisha kuwepo kwa makosa mbalimbali hususani iwapo mifumo ya lugha mbili husika ni tofauti. Lugha za Kinailotiki zina mfumo tofauti na ule wa Kiswahili ambayo ni lugha ya Kibantu. Makala haya yanaweka wazi athari za kifonolojia kutokana na lugha teule za Kinailotiki kwa Kiswahili tukizingatia michakato mitatu: Udondoshaji, uchopekaji na ubadilishaji wa fonimu.

Mapitio kuhusu Athari za Lugha ya Kwanza kwa ya Pili

Kwa mujibu wa Fromkin, Rodman na Hyams (2007), ujifunzaji wa lugha ya pili kwa watu wazima hutegemea mfumo wa kisarufi wa lugha yao ya kwanza. Baadhi ya makosa yanayojitokeza wakati wahusika hao wanapojifunza lugha ya pili hujikita katika uhamishaji wa kaida za kisarufi za lugha ya kwanza. Wanaisimu hawa wanaendelea kueleza kuwa athari ya lugha ya kwanza kwa lugha ya pili hudhihirika zaidi katika fonolojia, mofolojia na sintaksia. Wanatoa mifano ya athari ya lugha ya kwanza ambayo ni: Kwanza, Mjapani anayejiifunza Kiingereza kushindwa kutofautisha kati ya “write” na “light” kimatamshi kwa kuwa [r] na [l] si fonimu katika lugha yao; pili, Mwingereza, anayejiifunza Kiitaliano, kushindwa kubaini konsonanti ndefu na fupi ambazo hutumiwa kutofautisha maana za maneno katika lugha hiyo.

Akichunguza athari za lugha ya kwanza katika ujifunzaji wa lugha ya pili, Hagège (1999), anaeleza kuwa athari za aina hiyo hudhihirika miongoni mwa watoto na hata watu wazima. Anasisitiza kuwa athari huwa kubwa iwapo wahusika ni watu wazima kwa kuwa miundo ya lugha ya kwanza huzidi kuimarika umri unapoogezeka. Mtaalamu huyu anaendelea kuelezea kwamba, athari miongoni mwa watoto hupungua kadiri wanavyoendelea kujifunza lugha ya pili na kuna uwezekano wa athari hizo kuisha kabisa. Hagège (mtaje), anaongezea kuwa, mwalimu husika anapaswa kuelewa kwamba katika harakati za ujifunzaji lugha ya pili, mtoto huathiriwa na miundo ambayo anajua tayari kutokana na lugha ya kwanza.

Akishughulikia suala la kuathiriana kwa Kiswahili na lahaja ya Kitigania, Mukuthuria (2004), aligundua kwamba kuna matatizo mengi ya kiisimu yanayowakumba wanafunzi wanaotumia lugha ya Kitigania wanapojifundisha Kiswahili. Matatizo anayoyataja ni pamoja na yale ya kitahajia, kisarufi, uchanganyaji ndimi na kutafsiri dhana za Kiswahili kwa misingi ya Kitigania. Uchunguzi uliofanywa na msomi huyu ulithibitisha kwamba, chanzo cha matatizo hayo ni mifumo ya kifonolojia na kimofolojia ya lugha hizi.

Akichunguza athari za Ekegusii katika ujifunzaji wa Kiswahili, Mangwa (2005), anaeleza kuwa kulikuwa na makosa yaliyodhihirika katika matumizi ya Kiswahili ambayo yalikuwa na chanzo chake katika lugha ya kwanza (Ekegusii).

Aliendelea kueleza kuwa makosa yaliyogunduliwa yalichangia kuwepo kwa matokeo mabaya katika mtihani wa Kiswahili katika wilaya ya Kisii Kusini. Alieleza kuwa makosa hayo hujitokeza hasa katika hijai, sarufi na msamiati. Katika kuchunguza makosa husika, mtafiti huyu alitumia mijadala na uandishi wa insha kama chanzo cha data yake.

Bartoo (2004), akichunguza kuhusu ujifunzaji wa sintaksia ya Kiingereza wa wanafunzi wanaotumia Kikeiyo kama lugha ya kwanza, aligundua kuwa Kikeiyo kiliathiri mpangilio wa maneno katika sentensi za Kiingereza. Anasema kwamba, kutokana na tofauti za kimundo kati ya lugha hizo mbili, wanafunzi husika walihamisha muundo wa nje wa kisintaksia wa lugha yao hadi kwa lugha ya Kiingereza. Hali hii ilikuwa chanzo cha makosa aliyoyagundua mtafiti huyu katika mpangilio wa maneno katika sentensi zilizotungwa na watafitiwa hao.

Akishughulikia kuibuka kwa ‘Viswahili’ na utafiti wa Kiswahili, Munyua (2002), anasema kuwa athari za lugha ya kwanza kwa lugha ya pili husababisha makosa mbalimbali ya kimatumizi. Anaitumia dhana ya ‘Viswahili’ kurejelea matumizi potofu ya lugha ya Kiswahili kutokana na uhamishaji hasi kutoka kwa lugha mbalimbali za kwanza kama vile: Kibukusu, Ekegusii, Kikuyu, Kimeru, Kikalenjin na Dholuo. Alisisitiza kuwa athari husika hujitokeza katika viwango vyote vya lugha ambavyo ni: Fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Kuhusu idadi ya makosa katika tamko, Munyua (mtaje), alishikilia kuwa iwapo makosa ni mengi, tamko husika hukanganya; hivyo kutoeleweka. Alipendekeza kuwa tafiti zifanywe kuhusu ‘Viswahili’ kwa lengo la kuwaelekeza watunga mitaala ya Kiswahili kuzua mbinu mpya za ufundishaji wa Kiswahili sanifu.

Mudhune (1994) alichunguza ujifunzaji wa mofosintaksia ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa Kiluo kwa mtazamo wa Uchanganuzi Linganuzi. Anadai kuwa makosa kadha yaliyojitokeza katika kazi za wanafunzi husika yalitokana na athari za lugha yao ya kwanza (Dholuo). Hata hivyo, msomi huyo alisisitiza kuwa kulikuwa na makosa mengine yaliyogunduliwa na ambayo hayakuwa na chanzo chake katika lugha ya kwanza iliyotumiwa na wanafunzi waliochunguzwa. Mudhune (mtaje), alipendekeza kuwa tafiti nyingine zifanywe ili kuweka wazi vyanzo vya makosa mengine yanayojitokeza katika matumizi ya lugha mbali na yale yaliyo na chanzo chake katika lugha ya kwanza.

Lakkis na Malak (2000) walichunguza uhamishaji wa ujuzi kuhusu vihusishi uliofanywa na wanafunzi wa Kiarabu kutoka kwa Kiarabu hadi Kiingereza. Walizingatia uhamishaji chanya na hasi ili kuwasaidia walimu kutambua vipengele tata. Ugunduzi huu ungesaidia kuwaelekeza wanafunzi husika kuhusu wakati wa kutumia uhamishaji na wakati wa kutoutumia. Walihitimisha kuwa mwalimu ambaye lugha yake ya kwanza ilikuwa Kiarabu, alikuwa katika nafasi nzuri ya kutumia miundo ya vihusishi katika Kiarabu pale ambapo miundo hiyo iliafikiana na ile ya Kiingereza. Aidha, walimu husika walikuwa na wajibu wa

kuwaonyesha wanafunzi wao kuwa vitenzi na semi nyingine huambatanishwa na vihusishi kwa njia isiyoafikiana na miundo ya lugha yao ya kwanza.

Komunte (2001) alichunguza athari ya lugha za Kibantu katika ujifunzaji wa Kiingereza miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili nchini Tanzania. Anaeleza kuwa mazingira ya darasani yalitawaliwa na wingi-lugha ambapo wanafunzi wote waliochunguzwa walikuwa wakitumia lugha mbalimbali za Kibantu kama lugha zao za kwanza. Hali hii, kwa mujibu wa utafiti alioufanya Komunte (mtaje), ilichangia pakubwa ugumu uliodhihirika katika ujifunzaji wa lugha ya Kiingereza miongoni mwa wanafunzi husika. Kwa mujibu wa mchunguzi huyu, asilimia kubwa (82.9) ya wanafunzi ilikiri kuwa katika ujifunzaji wa stadi za kuzungumza na kusoma, ilifikiria katika lugha ya kwanza na kisha kuwasilisha dhana husika kwa Kiingereza. Mtaalamu huyo aligundua, pia, kwamba wanafunzi wengi hawakuwa na umilisi wa msamiati wa Kiingereza huku wengine wakitamka maneno ya Kiingereza kama yalivyoandikwa. Aidha, huku akitoa mifano ya fonimu mbalimbali za Kiingereza zilizotamkwa kwa njia isiyo sahihi, anabainisha kuwa lugha za kwanza ndizo zilizochangia katika utamkaji huo usiokuwa sahihi.

Katika uchunguzi wake kuhusu athari za lugha za kienyeji kwa Kiswahili katika eneo la Mara nchini Tanzania, Massamba (1986), aligundua kuwa lugha za kienyeji na lugha ya Kiswahili ziliathiriana. Mtaalamu huyu, hata hivyo, alijihusisha na jinsi lugha za kienyeji zilivyokiathiri Kiswahili katika viwango mbalimbali. Anaeleza kwamba, lugha husika zilikiathiri Kiswahili kifonolojia, kimsamiati na kisarufi. Katika fonolojia, Massamba (mtaje), anaonyesha jinsi sauti zilivyoongezwa au kudondoshwa katika matumizi ya maneno ya Kiswahili kutokana na athari ya lugha za kwanza, hali iliyosababisha makosa. Kuhusu msamiati, anaeleza kuwa maneno fulani kutoka lugha za kwanza za eneo la utafiti, yalipenyezwa na kutumiwa katika Kiswahili sanifu. Matokeo ya matumizi haya yalikuwa kuvuruga hali ya Kiswahili sanifu ambacho tayari kilikuwa na msamiati mwafaka wa kurejelea vitu au hali husika. Kwa upande wa sarufi, viambishi vilivyohamishwa kutoka lugha za kwanza na kuingizwa katika Kiswahili, vilisababisha makosa ya kimofolojia na yale ya kimuundo. Hali hii, kwa maoni ya mtaalamu huyu, ilikiuka kaida za Kiswahili sanifu; na hivyo, kutatiza uwasilishaji wa ujumbe ulionuiwa.

Kwa mujibu wa Ngugi (2007), lugha ya kwanza huathiri ujifunzaji wa lugha ya pili katika kiwango cha fonolojia. Katika kuchunguza namna lugha ya Kikuyu ilivyoathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili, mtafiti huyu aligundua kuwa athari husika zilijitokeza katika matamshi na pia katika hijai. Ngugi (mtaje), amesisitiza kwamba makosa mengi yaliyojitokeza katika matumizi ya lugha ya wanafunzi wa shule za upili waliotumiwa kama watafitiwa, yalitokana na uchopekaji, udondoshaji na unazalishaji. Ameeleza kwamba, mifanyiko hiyo ya kifonolojia ilidhihirika katika matumizi ya lugha ya wanafunzi husika huku makosa

yakijitokeza kutokana na tofauti katika mifumo ya lugha hizi mbili. Hatimaye, mtafiti huyu alipendekeza kuwa utafiti zaidi ufanywe kuhusu makosa ya kiswarufi, kimsamiati na kitahajia.

Mudhune (2008), alichunguza athari za kifonolojia kwa wasemaji wa Dholuo wanaojifunza Kiswahili. Aligundua kwamba kutofautiana kwa Kiswahili na Dholuo kifonolojia, kulisababisha makosa katika kipengele husika. Alieleza kuwa wakati wa ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili, wanafunzi wazawa wa Dholuo waliingiza kanuni za lugha yao ya kwanza katika Kiswahili. Athari kubwa ya kifonolojia aliyogundua mtafiti huyu, ilihusisha sauti ambazo zinapatikana katika lugha ya pili lakini zisizopatikana katika lugha ya kwanza.

Bosha (1993), alichunguza taathira za Kiarabu katika Kiswahili. Alijikita katika ukopaji wa maneno kutokana na Kiarabu na kuishilia kutumiwa katika Kiswahili. Aligundua kwamba asilimia 44.3 ya maneno yanayotumika katika Kiswahili yana chanzo chake katika Kiarabu. Anaendelea kueleza kwamba hali hiyo haiifanyi lugha ya Kiswahili kuchukuliwa kuwa Kiarabu, lahaja ya Kiarabu au pijini ya Kiarabu. Mtaalamu huyu anasisitiza kwamba hakuna lugha ambayo inaweza kukua kipweke kama kisiwa bila kuathiriwa wala kuathiri lugha nyingine.

Akichunguza uhusiano kati ya Kiswahili na Kihaya, Rubanza (1979), aligundua kuwa athari mbalimbali zilijitokeza katika matumizi ya Kihaya. Baadhi ya watafitiwa wa jamii-lugha ya Kihaya walitumia maneno ya Kiswahili katika kuwasilisha ujumbe wao ilhali dhana husika zingeweza kutajwa kwa kutumia maneno ya Kihaya. Wahojiwa katika utafiti huo walitoa sababu mbalimbali zilizowafanya watumie maneno ya Kiswahili mathalani: Hawakumbuki maneno mengine ya Kihaya wakati wa mawasiliano; na hivyo, kuwalazimisha kuyaingiza yale ya Kiswahili; maneno ya Kiswahili yaelekea kuwa na ushawishi mkubwa; na matumizi ya maneno ya Kiswahili yanalenga kufanya ujumbe wao ueleweke.

Mochiwa (1979), alichunguza athari ya Kiswahili kwa Kizigua (lugha inayozungumzwa katika wilaya ya Handeni, eneo la Tanga, Kaskazini Mashariki mwa Tanzania). Utafiti huo ulichunguza ujuzi wa lugha; ruwaza zilizojitokeza katika matumizi ya lugha, na mielekeo ya wanajamii kuhusu Kiswahili na Kizigua. Matokeo ya utafiti huo yalidhihirisha kuwa lugha ya Kiswahili iliathiri Kizigua katika viwango mbalimbali hususani kitamaduni, kisemantiki, na kileksika.

Mawazo ya wataalamu hawa wote yanaonyesha kuwa panapotokea mtagusano kati ya lugha moja na nyingine, kuathiriana huzuka. Imejitokeza wazi kuwa lugha za kwanza za Kiafrika huathiri lugha za pili hususani zile za kigeni na hivyo kusababisha makosa ya aina mbalimbali. Aidha, kunazo lugha za kigeni ambazo zimeathiriwa kwa mujibu wa wataalamu wengi kama vile Kiarabu kuathiri Kiingereza wakati wa ujifunzaji wa lugha ya pili. Ni kutokana na msingi

wa mawazo ya wataalamu hawa ambapo makala haya yanachunguza namna lugha mbalimbali za Kibantu zinavyoathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili.

Athari za Kifonolojia

Fonolojia ni taaluma ya isimu ambayo huchunguza ruwaza ya sauti na matumizi yake katika lugha mahsusi. Ni katika taaluma hii ambapo sauti hupangwa katika mfumo maalum kutegemea misingi ya lugha husika. Hapa ndipo tunapata lugha moja ikiathiri nyingine hasa ikiwa mifumo ya uundaji silabi ni tofauti. Hali hii huonekana kupitia kwa uhamishaji wa mifumo ya kifonolojia kutoka lugha ya kwanza hadi lugha lengwa kwa njia yenye kasoro. Matokeo yake huwa matumizi ya lugha kuwa na kasoro katika kiwango cha fonolojia. Michakato ya kifonolojia ambayo ilitumiwa na watafitiwa husika ni: Udondoshaji, uchopekaji na ubadilishaji wa fonimu katika maneno anuwai yaliyotumika katika insha tulizozichunguza.

Udondoshaji

Udondoshaji ni hali ya kuondoa kipashio katika neno kwa njia ambayo inakiuka taratibu za lugha husika. Tofauti katika utaratibu wa mfuatano wa sauti katika uundaji maneno kati ya lugha ya kwanza na ile ya pili, zilipelekea kudondoshwa kwa sauti au hata silabi nzima kwa njia iliyoleta kasoro katika maneno mbalimbali.

Tatizo la udondoshaji lilijitokeza katika insha zilizoandikwa na wanafunzi wazawa wa Dholuo. Mifano ya makosa ya aina hiyo inajitokeza katika jedwali linalofuata.

Jedwali 1: Makosa ya Udondoshaji katika Insha za Wanafunzi Wazawa wa Dholuo

Nambari	Udondoshaji	Sahihi
1	Tumeduwa [^] ...	Tumeduwaa ...
2	... akasema kuwa anajua mwanya Δ moja kwenye ua.	... akasema kuwa anajua mwanya m moja kwenye ua.
3	... wameji Δ ami wameji h ami ...
4	... Δ ivyo h ivyo ...
5	... ali Δ asha ali w asha ...
6	... kilichoku Δ a kilichoku w a ...
7	...ny Δ ele ny w ele ...

Asili: Ontieri (2010)

Katika mfano wa **1**, irabu /a/ imedondoshwa mwishoni mwa neno **tumeduwa**. Udondoshaji huu umetokana na hali kwamba ni nadra kwa maneno ya Dholuo kuishia kwa mkururo wa vokali (Mudhune 2008:98). Hivyo katika

mazingira ambapo neno lina mkururo wa vokali mwishoni basi mzawa wa Dholuo hudondoshwa moja ili kurahisisha matamshi. Katika neno **moja** (2), silabi {m} imedondoshwa. Katika lugha ya Kiswahili, konsonanti ng'ong'o /m/ huweza kujisimamia kama silabi iwapo kuna mkururo wa silabi {m}. Mpangilio kama huu haupatikani katika lugha ya Dholuo. Ili kurahisisha matamshi, wanafunzi wazawa wa Dholuo hudondoa silabi {m}. Hivyo basi, badala ya kutumia neno **mmoja** ili kuleta upatanishi wa kisarufi katika sentensi, mwanafunzi husika aliidondosha {m} iliyostahili kuwepo mwanzoni mwa kivumishi hicho. Katika mfano wa **3**, kumetokea udondoshaji wa konsonanti ya koromeo /h/. Kwa mujibu wa Mudhune (mtaje), hili kosa la udondoshaji wa /h/ hujitokeza katika matumizi ya lugha ya wazawa wa Dholuo. Mara nyingi /h/ inapotokea katikati mwa neno, hudondoshwa. Kasoro inayokaribiana na hiyo inajitokeza katika mfano **4** ambapo /h/ inadondoshwa na wazawa wa Dholuo inapotokea mwanzoni mwa neno. Hatimaye, katika mfano **5**, kiyeyusho/w/ kimedondoshwa katikati mwa neno. Mwanafunzi mzawa wa Dholuo hudondosha kiyeyusho hicho ili kurahisisha matamshi ya neno husika. Hali hii imehamishiwa kwenye maandishi kwa njia yenye kasoro kama inavyodhihirika katika neno **aliasha** ambalo kwa usahihi lilitakiwa kuwa **aliwasha**. Tatizo sawa na hili linajitokeza katika mifano **6** na **7** ambapo /w/ imedondoshwa katika maneno **kilichokua** na **nyele**.

Tatizo la udondoshaji lilijitokeza pia katika insha zilizoandikwa na watafitiwa wazawa wa Kikalenjin. Udondoshaji huu ulidhihirisha athari ya lugha ya kwanza ya watafitiwa husika. Mifano ya maneno yenye kasoro hiyo yanadhihirika katika jedwali linalofuata.

Jedwali 2: Makosa ya Udondoshaji katika Insha za Wabafunzi Wazawa wa Kikalenjin

NAMBARI	UDONDOSHAJI	SAHIHI
8	akawa [^] imiza	akawa h imiza
9	ali [^] ubiria	ali h ubiria
10	sitawa [^] i	Sitawa h i
11	sita [^] sahau siku	sita h sahau siku

Asili: Ontieri (2010)

Katika mifano **8**, **9** na **10**, herufi /h/ ndiyo imedondoshwa na hivyo kupelekea maneno husika kuwa na kasoro katika maendelezo. Herufi /h/ haipatikani katika Kikalenjin na hivyo watafitiwa waliidondosha pale ilipostahili kutumiwa. Nao mfano **11** unaonyesha jinsi watafitiwa mbalimbali walidondosha kirejeshi /i/ katika neno **sitasahau** ili kuonyesha urejeleo ambao ni muhimu katika Kiswahili sanifu. Kosa hili lilitokana na hali kwamba, maneno mengi ya Kikalenjin hayasheheni kirejeshi kama inavyotokea katika lugha za Kibantu ikiwemo Kiswahili. Tofauti hii katika maumbo ya maneno kati ya Kikalenjin na lugha za

Kibantu inaweka wazi sababu ya kosa hili kudhihirika katika insha nyingi zilizoandikwa na wanafunzi wa jamii-lugha husika.

Katika insha zilizoandikwa na watafitiwa wa Kimaasai, kosa la udondoshaji lilijitokeza. Kosa hilo lilijitokeza katika mfano ufuatao:

Udondoshaji	Sahihi
12* alitu \wedge arakisha	alitu \wedge arakisha

Katika mfano huu, mtafitiwa amedondosha fonimu /h/ katika neno husika. Fonolojia ya lugha ya Kimaasai haina sauti /h/ isipokuwa wakati ambapo inatokea katika sauti mwambatano /sh/. Mtafitiwa aliidondosha sauti hii kutokana na uzoefu wake wa lugha ya Kimaasai ambayo haina sauti hii. Aidha, ni muhimu kutaja hapa kuwa silabi ya mwisho katika neno husika **sha** haikumtatiza kwa kuwa inapatikana katika lugha yake ya kwanza.

Uchopekaji

Uchopekaji ni mchakato wa kifonolojia unaorejelea hali ambapo kipashio huongezwa katika neno. Matokeo ya hali hii ni kuvyazwa kwa neno ambalo linasheheni sauti ya ziada ambayo haikuwepo katika neno la kimsingi. Katika insha tulizozichanganua kulikuwa na makosa ya uchopekaji yaliyojitokeza ambayo yana msingi katika fonotaktiki ya lugha ya kwanza. Watafitiwa walitumia lugha zao za kwanza kama kielelezo kilichowaongoza katika kuendeleza maneno katika Kiswahili. Wanafunzi wazawa wa Dholuo walichopeka sauti kama inavyojitokeza katika jedwali linalofuata.

Jedwali 3: Makosa ya Uchopekaji katika Insha za Wanafunzi Wazawa wa Dholuo

NAMBARI	UCHOPEKAJI	SAHIHI
13	Matarajiyu	Matarajio
14	Baadala	Badala
14	Kuchukuwa	kuchukua
16	warejehe	warejee
17	Huamuzi	uamuzi

Asili: Ontieri (2010)

Katika mfano **13**, uchopekaji wa kiyeyusho /y/ umetokea ili kuvunja mwambatano wa irabu /i/ na /o/. Jambo hili hutokea kwa sababu katika lugha ya Dholuo ni nadra sana /i/ kufuatwa na /o/ (Mudhune, 2008). Uchopekaji wa /a/ katika mfano **14** umetokana na hali kwamba Dholuo ni lugha ambayo inasheheni irabu fupi na ndefu. Irabu ndefu katika Dholuo ni pamoja na /a/ katika **jatodo** (mpishi); /e/ katika **lem** (omba); /i/ katika **omit** (tamu); /o/ katika **kano** (kuweka), na /u/ katika **bul** (choma). Urefu wa irabu za Dholuo hutegemea vigezo mbalimbali kama vile mkazo na toni. Wanafunzi wazawa wa Dholuo huwa na mazoea ya kuongeza irabu katika maneno ya Kiswahili bila kukumbuka kuwa

lugha hii ina irabu fupi pekee. Kuchopekwa kwa kiyeyusho /w/ katika **kuchukuwa** kumetokea katika mfano **15** ili kuvunja mkururo wa irabu. Hapa pia kuna mfanyiko wa uyeyushaji ambapo /u/ inapofuatiwa na irabu nyingine yoyote isipokuwa hiyo yenyewe, kiyeyusho /w/ huvyazwa (Mukuthuria, 1997). Katika mfano huu, kiyeyusho /w/ kimeundwa kutokana na mfuatano wa /u/ na /a/. Hata hivyo, mtafitiwa ameutumia mfanyiko huo mahali pasipofaa na kuzalisha neno lisilokubalika katika Kiswahili sanifu. Katika mfano wa **16**, uchopekaji wa /h/ katika neno **warejehe** umefanywa ili kuvunja mfuatano wa irabu /e/. Katika fonotaktiki ya Dholuo, sauti hizi hazifuatani. Hatimaye, katika neno **huamuzi** (17), uchopekaji wa /h/ hutokea mwanzoni mwa neno iwapo kuna irabu moja au mbili katika mazingira hayo.

Ubadilishaji Fonimu

Tatizo la ubadilishaji wa fonimu lilijitokeza katika insha zilizoandikwa na watafitiwa wazawa wa Kikalenjin. Kati ya kasoro za kifonolojia, hili ndilo tatizo lililodhihirika zaidi katika insha za wanafunzi husika. Mifano inayoonyesha kasoro hii inajitokeza katika jedwali lifuatalo.

Jedwali 4: Makosa ya Ubadilishaji Fonimu katika Insha za Wanafunzi Wazawa wa Kikalenjin

NAMBARI	UBADILISHAJI	SAHIHI
18	mikuu niponye	miguu niponye
19	Kuboteza	kupoteza
20	Mazika	masika
21	Ujunguzi	uchunguzi
22	kujua saidi	kujua zaidi
23	chua la machweo	jua la machweo
24	uhapa	uhaba

Asili: Ontieri (2010)

Ubadilishaji unaodhihirika katika mifano hii (18 mpaka 24), umechangiwa pakubwa na ukosefu wa konsonanti anuwai katika Kikalenjin. Wakieleza kuhusu Kinandi (lahaja mojawapo ya Kikalenjin), Musau na Chacha (2001), wanasema kuwa lahaja hiyo haina konsonanti zifuatazo: /v, f, dh, th, d, g, b, h, z, sh, na gh/. Katika mfano **18**, matumizi ya /k/ badala ya /g/ yamesababisha dosari katika neno husika ambalo limeendelezwa kama **mikuu** ilhali mtafitiwa alistahili kuandika **miguu**. Kosa hili linatokana na ukosefu wa konsonanti /g/ katika Kikalenjin na hivyo kumfanya mwanafunzi husika kutumia /k/ ambayo inapatikana katika lugha hiyo ya kwanza. Aidha, /k/ hutamkwa kama [g] au [ɣ] katika Kikalenjin na hivyo athari ya matamshi hupelekea maendelezo yasiyokuwa sahihi. Tatizo linalokaribiana na hilo linajitokeza katika mfano **19** ambapo matumizi ya /b/

badala ya /p/ katika neno husika, yanatokana na athari ya matamshi. Wanavyoeleza Musau na Chacha (wataje), katika Kikalenjin, konsonanti /p/ hutamkwa kama [b]. Kasoro hii ndiyo imehamishiwa katika maandishi ambapo mtafitiwa aliandika **kuboteza** badala ya **kupoteza**. Katika mfano **20**, mtafitiwa ametumia /z/ ambayo haipatikani katika Kikalenjin badala ya /s/ ambayo ndiyo sahihi na inapatikana katika lugha hiyo. Hali hii imesababishwa na usahihishaji uliokithiri ambapo mtafitiwa anatumia konsonanti isiyo sahihi kutokana na kukanganywa na sauti husika (s na z) na kutojua ni wapi anatakiwa kutumia sauti ipi. Tatizo sawa na hilo linajitokeza katika mfano **21** ambapo mwanafunzi alitumia [j] ambayo haipatikani katika lugha yake ya kwanza katika nafasi ambapo alistahili kutumia [ʃ]. Katika mfano **22**, mtafitiwa ametumia /s/ ambayo inapatikana katika lugha yake ya kwanza badala ya /z/ ambayo haipatikani katika lugha hiyo. Matumizi haya ndiyo yanayosababisha upungufu unaodhihirika katika neno husika. Kasoro sawa na hii inajitokeza katika mifano **23** na **24** ambapo mtafitiwa ametumia [ʃ] badala ya [j] na /p/ badala ya /b/ kwa mfuatano huo. Mifano hii inaonyesha namna mwanafunzi alivyotumia sauti zisizostahili (ch na p) ambazo zinapatikana katika lugha yake ya kwanza katika nafasi ya sauti zilizostahili (j na b) ambazo hazipatikani katika lugha hiyo.

Mapendekezo

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, ni wazi kuwa wanafunzi wazawa wa jamii-lugha za Kinailotiki hudhihirisha athari mbalimbali za kifonolojia ambazo husababisha makosa katika uandishi wao wa Kiswahili sanifu. Hali hii inaweza kuepukwa kupitia kwa walimu husika kutambua kasoro hizi na kuwaelekeza wanafunzi namna ya kuziepuka. Itakuwa muhimu kusisitiza mfumo wa sauti katika Kiswahili sanifu huku mifumo la lugha husika za Kinailotiki ikiwekwa wazi hasa sauti zinazokinzana. Ni kupitia kwa juhudi hizi ambapo wanafunzi watahimizwa kufanya mazoezi kuhusu matumizi ya sauti zinazotatiza ili kuwa na umilisi wa kutosha kwa lengo la kuwawezesha kuyaendeleza maneno husika kwa njia sahihi.

Wadau mbalimbali hasa wakuza mitaala nchini Kenya wanapaswa kuzingatia vipengele vya kifonolojia ambavyo vinatatiza kutokana na matokeo ya utafiti huu. Msisitizo wa sauti tatanishi uwe msingi wa kushughulikia vipengele vya kifonolojia katika ngazi mbalimbali za elimu hususani katika shule za msingi na zile za upili. Juhudi hizi zitawawezesha wanafunzi husika kuimarisha matumizi yao ya lugha ya Kiswahili wanapoandika kazi mbalimbali.

Hitimisho

Makala haya yameshughulikia athari za kifonolojia zinazodhihirika katika uandishi wa insha miongoni mwa wanafunzi wazawa wa lugha mbalimbali za Kinailotiki. Athari zilizogunduliwa ni udondoshaji, uchopekaji na ubadilishaji wa

fonimu. Imedhihirika kuwa wakati ambapo wanafunzi wa jamii-lugha tatu walidondosha sauti katika maneno anuwai kimakosa, ni jamii-lugha moja iliyochopeka sauti au kubadilisha fonimu katika neno. Hivyo basi, ni wazi kuwa makosa kutokana na athari mbili za mwisho yalikuwa machache yanapolinganishwa na athari hiyo ya kwanza. Pia imebainika kuwa wanafunzi wa jamii-lugha za Kinailotiki waliotumiwa kama watafitiwa walitegemea mifumo ya kifonolojia ya lugha zao za kwanza wakati wa kuandika insha kwa Kiswahili. Hali hii ndiyo iliyochangia makosa anuwai ambayo tumeyachanganua katika makala haya.

Marejeleo

- Bartoo, J. P. (2004). *Acquisition of English Syntax by Keiyo L1 Speakers*. Tasnifu ya M.A (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.
- Bosha, I. (1993). *Taathira za Kiarabu katika Kiswahili pamoja na Kamusi Thulathiya*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Corder, S. P. (1967). The Significance of Learners Errors. Reprinted in J. C., Richards (Mh.). (1974, 1984). *Error Analysis: Perspectives on Second Language Acquisition*. London: Longman. Retrieved November 15, 2005 from <http://abisamra03.tripod.com/.../languagecq-erroranalysis.htm>.
- Fromkin, V., Rodman, R., & Hyams, N. (2007). *An Introduction to Language (8th ed.)*. Boston, MA: Thomson Wadsworth.
- Hagège, C. (1999). The Child Between Two Languages. In M. Karra, (2006). *Second Language Acquisition: Learners' Errors and Error Correction in Language Teaching*. Retrieved May 22, 2007 from <http://www.proz.com/doc/633>.
- Komunte, B. S. (2001). The Impact of Bantu Languages in English Language Learning Processes in Tanzania secondary schools. *Makala ya Kongamano la Kimataifa Kiswahili*, 2000, 287 – 296.
- Lakkis, K. na Malak, M. A. (2000). Understanding the Transfer of Prepositions. *Forum*, Vol 38, No3. Retrieved May 22, 2007 from <http://exchanges.state.gov/forum/vol38/no3/p26.htm>.
- Mangwa, D. O. (2005). *Athari za Ekegusii katika Kiswahili na Zinavyochangia Matokeo Mabaya ya Mtihani wa Kitaifa wa Kiswahili kwa Wanafunzi Wakisii wilayani Kisii Kusini*. Tasnifu ya M.A (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.
- Massamba, D. P. B. (1986). On the Influence of Local Languages on Kiswahili: The Case of Mara Region in Tanzania. *Kiswahili*, 53/1 na 53/2, 67-83.
- Mudhune, E. S. (1994). *A Contrastive Analysis Approach to the Learning of Swabili Morphosyntax by Luo Speakers*. Tasnifu ya M.A. (Isiyochapishwa). Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya.

- Mudhune, D. R. (2008). *Athari za Kifonolojia kwa Wasemaji wa Dholuo Wanaojifunza Kiswahili*. Tasnifu ya M. A. (Isiyochapishwa). Nakuru: Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.
- Mukuthuria, M. (1997). *Njeo katika Kitenzi cha Kitigania*. Tasnifu ya M. A. (Isiyochapishwa). Nakuru: Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.
- _____ (2004). *Kuathiriana kwa Kiswahili na Kimeru: Mfano kutokana na Wanafunzi wa Kitigania, Kenya*. Tasnifu ya PhD (Isiyochapishwa). Nakuru: Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.
- Munyua, J. G. (2002). The Emerging Viswahili and Kiswahili Research. Katika K. I. Simala (Mh.) *Utafiti wa Kiswahili* (uk. 97 – 107). Eldoret: Moi University Press.
- Musau, P. na Chacha, L. (2001). *Mbinu za Kisasa za Kufundishia Kiswahili kwa Walimu wa Shule za Msingi, Upili, na Vyuo*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Ngugi, J. K. (2007). *Uchunguzi wa Taathari za Kifonolojia miongoni mwa Wanafunzi Wagikuyu: Mfano kutoka Tarafa ya Bahati, Nakuru*. Tasnifu ya M. A. (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.
- Richards, J. C. (1974). Error Analysis and Second Language Strategies. In J. H. Schumann and N. Stenson (Wah.), *New Frontiers in Second Language Learning*. Rowley, Mass.: Newbury House.
- Rubanza, Y. I. (1979). *The Relationship between Kiswahili and other African Languages: The Case of Kihaya*. Tasnifu ya M. A. (Isiyochapishwa). Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.